AAP 68 (2001) - Swahili Forum VIII • 67-79

NAFASI YA KISWAHILI KATIKA LUGHA YA ALAMA YA TANZANIA[1]

A. Y. MRETA NA H. R. T. MUZALE

Sign language in Tanzania is a relatively new field of linguistics that is yet to attract many researchers and linguists in particular Tanzanian Sign Language (TSL) functions as a unifying tool for the deaf in the country and, probably, beyond. This language, which is still at its early stage of development, is used in the same linguistic environment with Kiswahili, the national language, which is more established. The situation leaves TSL disadvantaged and is thus likely to cause a one-way linguistic influence, from Kiswahili to TSL. This paper, therefore, examines the nature and impact of the situation. Firstly, it focuses on the question of whether or not TSL is an independent language that has developed as a separate language, quite distinct from the spoken languages of the communities that surround it, especially Kiswahili. Secondly, it examines the extent to which Kiswahili has influenced TSL and thus the role that the former plays in learning and developing the latter. The results of the study show that Kiswahili has had some influence on TSL but the influence is marginal at lexical level. Of all the signs studied, only 13% were directly related to Kiswahili. The majority of the signs studied were found to be iconic in nature, but only 12% of all signs were semantically transparent. Even in these cases where the signs are transparent, the transparency of the signs is not based on one's knowledge of Kiswahili. Most of the transparent signs are common gestures that any person of any ethnic origin can interpret. The study has thus established that TSL is more of a sign language than signed language. It is an indigenous African sign language, unrelated to the Western Sign Languages, except for the manual alphabet. Finally, the study predicts that much of the transparency and iconicity in TSL will gradually fade away as the language develops across time, space, and generations.

Utangulizi

Makala haya yanatoa muhutasari wa utafiti wa Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) uitwao 'The influence of Kiswahili on Tanzanian Sign Language' ambao ulifanywa na A.Y. Mreta na H.R.T. Muzale, wote wa Idara ya Lugha za Kigeni na Isimu, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, kati ya 1999 na 2000, kwa kugharimiwa na SIDA/SAREC. Utafiti huo ulikuwa na malengo makubwa mawili: a) kuchunguza kama LAT ni lugha huru, inayojitegemea na bila kuathiriwa na lugha zinazoizunguka (kama vile Kiswahili) ama lugha za mataifa mengine; b) kutathmini na kuona kama LAT imeathiriwa na Kiswahili kwa mantiki ya kwamba ujuzi wa mtu katika Kiswahili unamsaidia kuelewa au kujifunza LAT kwa haraka na mafanikio zaidi.

Makala haya yamejikita zaidi kwenye lengo kuu la pili la utafiti huo. Kwanza yamejaribu kuona kama Kiswahili kina mchango wowote katika uundaji wa alama mbali mbali za LAT. Pili, yameangalia kama alama zilizopo zinahusiana moja kwa moja na Kiswahili kwa njia mbalimbali kama vile alama zitokanazo na tafsiri-mkopo (loan translation), alfabeti, kuashiria

[1] Makala haya yalisomwa katika Kongamano la Kiswahili la 14 Chuo Kikuu cha Bayreuth, Ujerumani tarehe 25–27 Mei, 2001.

matamshi ya neno kwa midomo, au hazihusiani kabisa. Kwa upande huo, makala yametazama pia swala la uangavu wa alama husika. Makala yamelenga kubainisha kiwango cha mahusiano kati ya kiashiria na kiashiriwa, yaani, ni kwa upeo gani maana ya alama inakuwa wazi kwa mtazamaji hata kama hajui LAT. Tatu, makala yameelezea kama kuna ukweli wowote kuwa ujuzi na maarifa katika Kiswahili kwa viziwi kunachangia katika uundaji wa alama za LAT. Kwa ujumla, makala haya yamedhamiriwa kujenga msingi wa kuchambua na kufafanua LAT katika mazingira ya lugha kadhaa zinazoizunguka jamii ya viziwi, na hivyo kuona kama LAT ina uwezo wa kuhimili yenyewe pasipo Kiswahili.

1. Jamii ya Viziwi Tanzania

Inafahamika kuwa jamii ya viziwi ni jumuiya ya watu wenye utamaduni wao, lugha yao wenyewe, uzoefu wao wa kimaisha pamoja na matashi yanayofanana. Lakini kwa upande wa Tanzania, mpaka sasa kuna kikwazo kikubwa kinachoikumba jamii ya viziwi nacho ni lugha.[2] Viziwi walio wengi wamejikuta katika hali ya kulazimika kujifunza na kutumia lugha iliyopo katika mazingira yao, kama vile, lugha za kijamii zitumikazo nyumbani au vijijini, pamoja na Kiswahili ambacho wengi wao hujifunza hasa wanapokuwa shuleni. Matokeo yake, viziwi huanza kutumia lugha za mazungumzo, zinazowahitaji kutumia ala za sauti, wakingali wadogo. Pamoja na hilo, walio wengi hutengwa na jamii katika mazungumzo, wakiitwa bubu, na hivyo kuishi bila kuwa na mawasiliano na jamii waishimo. Kwa msingi huo, kunakosekana pia mawasiliano kati ya kiziwi mmoja na viziwi wengine waishio katika vijiji au miji ya jirani. Isitoshe, idadi ya viziwi ni ndogo mno vijijini ambako ndiko kuna wananchi walio wengi. Mwenendo huo husababisha kutokuwepo kwa viziwi wanaojifunza lugha ya alama kama lugha yao ya kwanza. Hata hivyo, viziwi wanapokutana, hasa shuleni, hubuni na kuunda alama ambazo huzitumia katika kuwasiliana wenyewe kwa wenyewe. Tatizo kubwa ni kwamba mpaka sasa lugha yao ya alama bado haijatumiwa kama lugha sanifu ya kuwafundishia viziwi katika shule zao zilizopo nchini. Matokeo yake ni kwamba inakadiriwa kuwa ni asilimia moja tu ya viziwi katika Tanzania ambao wanapata nafasi ya kutumia LAT bila kikwazo chochote, kwa mujibu wa taarifa ya Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA, 1993). Hali hii inadhihirisha umuhimu wa utafiti, kuiendeleza, kuisambaza, na kuiimarisha zaidi LAT.

2. Historia fupi ya Lugha ya Alama ya Tanzania

Kulingana na ufahamu wetu ni kwamba ni tafiti tatu tu ambazo kwa njia moja ama nyingine zimejihusisha na matatizo ya viziwi au LAT. Tafiti hizo zimefanywa na CHAVITA (1993), Possi (1999) na Mreta na Muzale (1999). Katika utafiti wa kwanza CHAVITA walifanya

[2] Inakadiriwa kuwa idadi ya viziwi Tanzania inafikia laki tano. Lakini ni vigumu sana kupata taarifa ambazo ni sahihi kwa sababu hakujafanyika sensa ya kuhesabu viziwi katika Tanzania.

juhudi za kutafiti na kukusanya alama mbalimbali zitumiwazo na viziwi kutoka mikoa mbalimbali nchini Tanzania. Matokeo ya utafiti huo ni haya yafuatayo:

i. Ilizaliwa lahaja sanifu ijulikanayo kama Lugha ya Alama Tanzania (LAT).

ii. Ilitengenezwa kamusi ya kwanza ya Lugha ya Alama Tanzania na kusambazwa katika shule zote za viziwi.

iii. Wakalimani wa kwanza wa LAT waliandaliwa na kupewa mafunzo ya ukalimani na mbinu za mawasiliano.

Kutokana na juhudi hizo, kwa sasa wakalimani wanaonekana kwenye baadhi ya vipindi vya runinga (TV) wakikalimani ujumbe wa vipindi hivyo kwa viziwi. Hata hivyo, vipindi vilivyo vingi bado havijapata wakalimani kutokana na sababu mbali mbali.

Utafiti wa Possi (1999) ulidokeza kuwa ukosefu wa mfumo maalumu wa elimu ya viziwi umekuwa ukiwafanya viziwi wafundishwe kwa lugha tofauti katika kila hatua walizopitia. Kwa mfano, wamekuwa wakianza na lugha za kijamii katika mazingira ya nyumbani, halafu Kiswahili katika shule za msingi, na kisha Kiingereza katika sekondari. Kwa hali hiyo, mtafiti huyu alipendekeza kuwa Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia wanafunzi viziwi kwenye shule za sekondari badala ya Kiingereza.

Utafiti wa tatu ulichambua matatizo mbalimbali ya kiisimu, kielimu, na kijamii yanayoikabili jumuiya ya viziwi nchini. Yafuatayo ni baadhi ya matatizo hayo.

i. Kuna upungufu mkubwa wa zana na vifaa vya kielimu.

ii. Viziwi walio wengi hawajawahi kukutana na viziwi wengine.

iii. Viziwi walio wengi huishi kipweke katika jamii zao, wakijaribu kuwasilisha mahitaji yao muhimu kwa wanaosikia kwa kutumia lugha ya mazungumzo.

iv. Viziwi hawatambuliwi au kuthaminiwa inavyostahili.

v. Hakuna mpango wowote wa kuwatambua watoto wenye matatizo ya kusikia katika ngazi za vijijini, ili kuwapa huduma inayostahili toka mwanzo.

vi. Hakuna mpango wowote maalum kwa ajili ya watoto wenye matatizo ya kusikia.

vii. Wazazi na walezi wa watoto viziwi hawana ujuzi wowote katika LAT.

Kutokana na yaliyoelezwa hapo juu, ni dhahiri kuwa huu ni mwanzo tu, bado tafiti nyingine nyingi kuhusu LAT na Jumuiya nzima ya viziwi zinahitajika sana. Katika utafiti huu wa sasa, uchunguzi wa mwanzo tulioufanya juu ya LAT ulionyesha kuwa alama nyingi zinazotumiwa zina sababu fulani zilizochangia kuteua au kuziunda alama hizo. Kwa upande mmoja, utambuzi wa namna hiyo unapingana na maana nzima ya unasibu ambao kwa muda mrefu umekuwa kigezo muhimu katika kuelezea maana ya lugha. Lakini kwa upande mwingine, utambuzi huo ulionekana kukubaliana kabisa na uchunguzi wa utanakali katika Lugha ya Alama ya Marekani (ASL), ambayo mwanzoni alama zake nyingi zilikuwa angavu na bayana kimaana.

Hata hivyo, tafiti za hivi karibuni zimedhihirisha kuwa alama za ASL kwa sasa zimepoteza ule uangavu wake wa mwanzo. Kwa hiyo, lugha ya alama inaweza ikaanza na alama angavu, bayana, na tanakali ambazo baadaye hupoteza sifa hizo kutokana na mabadiliko ya kihistoria na kijamii katika jumuiya. Utafiti huu pia umedhamiria kuona kama hali hiyo inapatikana pia kwenye LAT. Swali mojawapo la msingi lililoshughulikiwa katika utafiti huu lilikuwa: "Alama za LAT ni angavu kiasi gani katika swala la kubainisha maana ya alama hizo kwa misingi ya uhusiano baina ya kiashiria na kiashiriwa? Hilo na mengine, yatajadiliwa katika vifungu kadhaa huko mbele.

3. Mbinu zilizotumiwa katika utafiti

3.1. Uteuzi wa Vituo

Utafiti huu ulifanyika katika awamu kuu mbili. Awamu ya kwanza ilifanyika jijini Dar-es-Salaam, kwa kuhusisha makao makuu ya CHAVITA (Mtoni) na shule ya viziwi Buguruni. Awamu ya pili ilifanyikia katika Shule ya Viziwi Mwanga, mkoani Kilimanjaro. Vigezo vitatu vilitumika katika kuchagua vituo hivyo, ambavyo ni: a) historia ya vituo husika, b) ushiriki na kujihusisha kwa vituo hivyo katika maswala ya LAT, na c) upatikanaji wa data katika vituo hivyo.

Kwa upande mmoja, makao makuu ya CHAVITA ndipo penye taarifa za msingi na nyaraka muhimu zinazotoa historia fupi ya LAT na maendeleo yake tangu kuzaliwa kwake. Shule ya msingi Buguruni ina historia ndefu kuhusiana na elimu ya Viziwi, pamoja na ukweli kwamba shule hii ipo katika jiji lililo kubwa kuliko yote nchini, tofauti na shule za vijijini au kwenye miji midogo.

Kwa upande mwingine, Shule ya Viziwi Mwanga ilijihusisha na tafiti za mwanzo za LAT hasa katika kutengeneza Kamusi ya kwanza ya LAT. Zaidi ya hapo, shule hiyo ipo mbali na Dar-es-Salaam, kwa hivyo vituo hivi viwili haviwezi kuathiriana kirahisi, hasa kwa kuchukulia kinadharia kuwa lugha za alama za maeneo hayo kuwa ni lahaja tofauti za LAT. Pamoja na hayo, uongozi wa vituo vyote hivyo vitatu ulishaafiki na na kuanza kuhamasisha matumizi ya LAT. Kwa vile nia ya utafiti ilikuwa ni kuangalia matumizi ya lugha ya alama, hatukuweza kuteua shule nyingine za viziwi kama vile Tabora ambayo uongozi wake ulikuwa bado ukisisitiza sana matumizi ya kusoma midomo badala ya kutumia lugha ya alama.

3.2. Upatikanaji wa Watafiti wasaidizi

Utafiti huu ulifanywa na watafiti wakuu wawili na watafiti wasaidizi kadhaa. Kigezo kilichotumiwa kuwapata wasaidizi hao kilikuwa ni kuangalia watu wenye uzoefu kukusanya data za lugha ya alama au wenye uzoefu wa ukalimani katika lugha hiyo, pamoja na kuvifahamu fika vituo vya utafiti huu. Mmoja wa watafiti wasaidizi hao katika kila kituo alikuwa mkalimani, ili kurahisisha na kufanikisha mawasiliano hasa kati ya watafiti wakuu na wenyeji wao.

Kazi kubwa ya watafiti wasaidizi ilikuwa kueleza na/ama kujaribu kuwadadisi viziwi watafitiwa ili kupata taarifa kuhusu alama mbalimbali. Taarifa zilizodadisiwa na ambazo zilihitajika ni chanzo au asili ya alama mbalimbali. Kwa hivyo vitomeo na misemo mbalimbali kutoka katika *Kamusi ya Lugha ya Alama ya Tanzania* vilitumiwa.

3.3. Jinsi ya kukusanya data

Ukusanyaji wa data ulifanywa katika hatua tatu kama zitakavyooneshwa hapa chini.

3.3.1. Kutoa visawe vya alama za vitomeo

Watafitiwa walitakiwa kutoa visawe vya alama za vitomeo 500 kutoka kwenye Kamusi ya Lugha ya Alama. Zoezi hilo la visawe lilifanywa mara mbili, yaani, mara ya kwanza Dar-es-Salaam na baadae Mwanga. Zoezi lililofanyikia Dar-es-Salaam lilichukuliwa katika picha za video, ambapo zoezi la Mwanga liliangalia zaidi tofauti zilizojitokeza kutokana na utafiti wa Dar-es-Salaam, kwa hivyo zilichukuliwa picha za kawaida tu.

3.3.2. Chanzo / Asili ya Alama

Ili kujua asili ya kila alama, viziwi waliulizwa kuhusu chanzo, chimbuko, au asili ya alama wanazozitumia. Jambo moja lililojitokeza wazi ni kwamba alama nyingi zilikuwa na sababu ya kuchaguliwa au kuundwa kwake. Na viziwi walisisitiza kwamba alama haiwezi kuwa nasibu kabisa kwa sababu kabla ya kuunda alama yoyote ile ni lazima kufikiria vigezo mbalimbali. Kwa maneno mengine, alama inaundwa kutokana na kuhusisha dhana inayodhamiriwa na kitu au hali fulani katika mazingira ya viziwi. Kwa msingi huo, ingetegemewa kwamba kiwango cha unasibu katika alama kingekuwa chini, wakati kiwango cha ubainifu wa maana ya alama hizo kingekuwa juu, kwa vile alama hizo zinaashiria vitu au mambo yaliyo katika jamii waishimo viziwi na watu wanaoongea. Hata hivyo, haikuwa rahisi kwa viziwi kuelezea chanzo cha kila alama iliyotafitiwa. Sababu kubwa ni kwamba alama zeneywe zina vyanzo na asili tofauti. Kwa mfano, baadhi ya alama zilikopwa kutoka katika lugha nyingine za alama za mikoani na nyingine kutoka nje ya Tanzania, kama vile Finland. Kwa hivyo haikuwa rahisi kuchambua alama za aina hiyo ambazo waanzilishi wake hawakuwa karibu ili kutoa ufafanuzi. Zilikuwepo pia alama za kienyeji ambazo chimbuko lake halikuweza kufahamika mara moja kwa vile viziwi wahusika walikwishasahau chanzo chake.

3.3.3. Majadiliano

Utafiti huu ulihusisha pia majadiliano ya aina tatu. Kwanza, yalifanyika majadiliano baina ya watafiti na viziwi kwa kila kituo cha utafiti. Katika majadiliano hayo, viziwi walitoa taarifa kuhusu chanzo au asili ya alama mbalimbali pamoja na matumizi ya alama hizo miongoni mwao. Vile vile, majadiliano yalihusu taarifa nyingine za LAT kama vile kusambaa kwake mashuleni, mijini, na nyumbani, pamoja na matumizi yake baina ya viziwi wa sehemu moja na wale wa sehemu nyingine.

Aina ya pili ya majadiliano ilikuwa kati ya watafiti na wakalimani wa LAT. Katika mahojiano hayo, wakalimani walitoa taarifa kuhusu uzoefu wao katika kutumia na kufasiri LAT, na jinsi wanavyowasiliana na viziwi. Walielezea pia kuhusu mbinu mbalimbali wanazotumia katika kukabili alama au dhana mpya, pamoja na matatizo yao binafsi yahusuyo umahiri wa lugha tatu (Kiswahili, Kiingereza, na LAT), na yale yatokanayo na viziwi wasio na uzoefu wa kutosha katika kuitumia LAT.

Aina ya tatu ya majadiliano ilielekezwa kwa walimu katika shule za viziwi. Baadhi ya walimu hao kutoka shule mbili za utafiti (Buguruni na Mwanga) walikuwa viziwi pia. Majadiliano hayo yalilenga zaidi kujua uzoefu wa walimu hao katika kuwafundisha viziwi, na pia matatizo mbalimbali wanayokabiliana nayo, katika mazingira yenye mchanganyiko wa matumizi ya Kiswahili na LAT.

4. Matokeo ya Utafiti

4.1. Chimbuko / Asili ya Alama za LAT

Alama zote zilizotafitiwa ziliweza kuainishwa katika makundi makubwa manne, nayo ni:

a) Alama zenye asili ya Kitanzania,

b) Alama zilizokopwa (i.e., zenye asili ya kigeni)

c) Alama za alfabeti

d) Alama ambazo asili yake haifahamiki

Utafiti umeonyesha kuwa alama zilizo nyingi zipo katika kundi la kwanza, yaani, zimeundwa na viziwi kutoka sehemu mbalimbali nchini mwao. Alama za kundi hili zimegawanyika tena katika makundi makubwa mawili. Kwanza ni alama za LAT (ambazo viziwi, hasa wa mikoani, huzitaja kama "alama za CHAVITA", na pili ni alama za mikoani ambazo huhusishwa na makundi mbalimbali kama vile shule za viziwi Buguruni na Mwanga. Jambo moja la kuvutia ni kwamba viwizi kutoka makundi hayo mawili (i.e., kundi la "alama za CHAVITA" na wale wa mikoani) wanapokutana wanawasiliana kwa kuchanganya alama hizo na wakaweza kueleweana.

Mgawanyo wa alama hizo ni kama ifuatavyo:

a) Alama zenye asili ya kitanzania ni 90% ya alama zote zilizotafitiwa.

b) Alama nyingine zote zilizobakia ni 10% tu. Mgawanyo wake ni kama ifuatavyo:

   i) Alama za alfabeti (ambazo hususani huhusisha herufi ya kwanza ya neno) ni 5%;

   ii) Alama zilizokopwa kutoka lugha nyingine za alama nje ya nchi ni 3%;

   iii) Alama ambazo asili yake haifahamiki ni 2%.

4.2. Unasibu wa Alama za LAT

Katika jaribio la unasibu na utanakali wa alama husika tulipata matokeo yafuatayo. Ni alama chache tu ambazo hazina utanakali. Alama hizo zinaweza kutambuliwa kama alama nasibu kwa msingi wa kwamba hazina mahusiano ya moja kwa moja baina ya kiashiria na kiashiriwa. Jumla ya alama hizo ilifikia asilimia 10% tu ya alama zote. Hata hivyo, tunafikiri kwamba kiwango hicho cha asilimia kingekuwa chini zaidi kama tungeweza kupata asili ya alama zote zilizotafitiwa. Ugumu wa kufuatilia asili ya alama zote unatonana hasa na kutokuwepo kwa taarifa za kietimolojia za lugha husika na alama zake. Jambo hilo linaibua changamoto ya kuanza kuweka kumbukumbu za maendeleo na ukuaji wa LAT.

Alama nyingine zote zilizobakia ni tanakali. Kati ya hizo, nyingine ni ishara tu za kawaida ambazo hutumiwa pia na wasio viziwi katika mawasiliano yao ya kila siku. Alama hizo zimeainishwa katika makundi mawili yafuatayo. Kundi la kwanza ni la alama tanakali zilizo dhahiri, ambazo ni 40%. Kwa mfano zipo alama za vitenzi k.v., *ku-la, ku-nywa, ku-lima,* na *ku-kimbia*; nomino, k.v., *saa, kamera,* na *uso*; misemo mbalimbali k.v., *kwaheri, tafadhali, subiri,* na *asante*. Alama kama hizo ni rahisi kwa mtu yeyote kuelewa maana yake bila kuuliza. Kundi la pili ni alama tanakali zisizo dhahiri, ambazo ni 50%. Katika kundi hili la alama tanakali zisizo dhahiri tunakuta alama zile ambazo huashiria kitu fulani lakini humaanisha kitu kingine. Swala muhimu hapa ni kwamba kunakuwepo na mahusiano ya aina fulani baina ya kiashiria na kiashiriwa, kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 1 hapa chini.

Jedwali 1:

	alama inayoonyeshwa	maana yake	maelezo
1.	kuchuma chai	Mkoa wa Mbeya	Watu wa mkoa wa Mbeya hulima chai.
2.	kusukuma	Wasukuma	Neno "wasukuma" limedhaniwa kuwa linatokana na mzizi wa kitenzi "ku-sukuma".
3.	dole gumba kuonyesha nyuma kupitia juu ya bega	jana	Kupunga kuelekea nyuma ina maana "past" "wakati uliopita".
4.	kofia	Mwislamu	Waislamu huvaa sana kofia.
5.	ziwa	mwanamke/mke	Ziwa ni kuwakilishi au kitambulisho cha mwanamke.

4.3. Chimbuko la maana za alama

Katika uchambuzi wa kisemantiki uliofanyika, tuliweza kuziainisha alama katika makundi makuu matatu ambayo ni alama zitokanazo na "tafsiri-mkopo", alama za uwakilishi, na alama nyinginezo. Msemo wa "tafsiri mkopo" umetumika hapa ukiwa na maana ya kutafsiri maneno/au misemo ya Kiswahili na jinsi inavyofasiriwa kulingana na utambuzi wa viziwi wa maneno au dhana husika. Tazama mifano ifuatayo hapo chini.

Jedwali 2:

	neno	**tafsiri-mkopo/ au tafsiri ya viziwi**	**alama na maana ya ndani**
6.	Tabora *(mkoa/mji)*	kutokana na maneno mawili ya Kiswahili: **taa** + **bora**	hutoa alama yenye sehemu mbili: "taa" + "bora"
7.	Mara *(mkoa)*	kutokana na neno la Kiswahili **mara** lenye maana ya "kuzidisha"	huchora alama ya "X" (hewani)
8.	Wahaya *(kabila)*	kutokana na neno la Kiswahili: **haya**	hufunika uso kwa kiganja kuashiria "haya/aibu"
9.	Wasambaa *(kabila)*	kutokana na kitenzi cha Kiswahili: **ku-sambaa**	huashiria tendo la "ku-sambaa" kwa kutumia mkono mmoja
10.	juzi	kutokana na tafsiri ya **jana ya jana**	huelekeza kidole gumba nyuma juu ya bega (vidole vingine vikiwa vimekunjwa) mara mbili kuashiria "jana mara mbili"

Kwa upande mwingine alama za uwakilishi ni zile zinazowakilisha kitu. Mifano ifuatayo (Jedwali 3) itasaidia kuelezea zaidi dhana hiyo.

Jedwali 3:

	neno	**alama**	**maana**
11.	Wagogo	kugusa paji la uso kwa kidole cha shahada	Wagogo huweka "alama kwenye paji la uso"
12.	Kilimanjaro	mlima wenye theluji juu yake	"mlima Kilimanjaro"
13.	Zanzibar	kofia	kuna "Waislamu wengi" Zanzibar
14.	gereza	pingu	"kukamatwa/kufungwa jela"
15.	kanisa	msalaba	alama ya kawaida inayowakilisha "kanisa"

4.4. Uangavu

Ingawa utafiti unaonyesha kuwa alama nyingi ni tanakali, hali hiyo haimaanishi kuwa ni lazima alama hizo ziwe angavu na wazi kwa mtazamaji. Ukiondoa ishara za kawaida ambazo kila mtu anazitumia katika mawasilianao ya kila siku, sio rahisi kwa mtu (ambaye hana uelewa wowote katika LAT) kuweza kumwangalia kiziwi akitumia lugha hiyo na kutambua maana ya alama zinazotumika. Kwa hiyo, alama nyingi siyo angavu; Utafiti huu umeonyesha kuwa 88% ya alama zilizotafitiwa siyo angavu, kama inavyodhihirishwa na majedwali yote matatu hapo juu. Inambidi mtu awe anaijua LAT ili kuweza kutambua maana ya alama zake.

4.5. Uhusiano baina ya Kiswahili na Alama

Jambo jingine lililobainika kutokana na uchambuzi wa alama hizi ni kwamba ni alama chache tu ambazo zina uhusiano wa moja kwa moja na Kiswahili. Kwanza tueleze tunamaanisha nini tunaposema 'uhusiano wa moja kwa moja na Kiswahili'. Hapa tunazungumzia alama zile zote ambazo ziliundwa kwa misingi ya kutegemea zaidi ujuzi na maarifa ya kiziwi katika Kiswahili. Yaani, Kiswahili kimechangia kwa njia moja au nyingine katika kuziunda alama hizo, kutokana na matumizi ya Kiswahili miongoni mwa viziwi. Uchambuzi wa alama hizo unaonyesha kuwa alama ambazo zilikuwa na uhusiano huo wa moja kwa moja na Kiswahili zilikuwa asilimia 13% tu. Katika alama za vitomeo zilizochambuliwa ambazo zilihusiana na Kiswahili, ziliweza kubainishwa katika makundi matatu yafuatayo. Kundi la kwanza ni la alama zinazohusisha alfabeti, hasa herufi ya kwanza ya neno husika. Karibu alama zote za aina hii zimeundwa kwa alama ya herufi ya kwanza ya neno la Kiswahili. Wakati mwingine herufi hiyo huambatana na alama nyingine ambazo kwa pamoja huunda alama tata. Kundi hili ni kubwa zaidi kuliko hayo makundi mengine, yaani 38.5% ya alama zote zenye uhusiano wa moja kwa moja na Kiswahili. Tazama mifano ya alama hizo katika Jedwali hapa chini.

Jedwali 4:

	neno	alama	maelezo ya ziada
16.	**k**aka	**K**	Alama "**K**" huundwa karibu na mdomo, ikiambatana na midomo kutamka neno "**kaka**".
17.	**b**inamu	**B**	Alama "B" huundwa karibu na shavu, ikiambatana na midomo kutamka neno "**binamu**".
18.	**T**anzania	**TZ**	Zipo alama nyingine kadhaa kwa neno hilo.
19.	**U**ganda	**U**	Alama hii husaidiwa zaidi na muktadha wa matumizi yake.
20.	**J**umatatu	**J3**	Baadhi ya siku za wiki huwa na alama zenye muundo, k.m., Jumanne > **J4** na Jumatano > **J5**.

Kundi la pili linaundwa na alama zilizotokana na tafsiri mkopo kutoka kwenye dhana za Kiswahili. Hizi ni 32.3% ya alama zote zenye uhusiano wa moja kwa moja na Kiswahili. Hata hivyo, kwa kuzingatia mifano ya alama zilizotolewa katika Jedwali 2 hapo juu, imedhihirika kuwa wakati mwingine tafsiri hizo zinakuwa na hitilafu kwa sababu siyo sahihi. Hapa tunazungumzia alama kama "Tabora" ambayo imekopwa na kutafsiriwa kama muungano wa maneno mawili: "taa" na "bora". Hata hivyo, alama zinazoundwa kwa mtindo huu nazo zinakidhi haja ya watumiaji kama nyingine zote, bila kujali au kuathiriwa na kasoro za chimbuko au asili yake.

Kundi la tatu ni la alama zinazoundwa na kufanywa kwa kutumia midomo. Mifano mizuri ya alama hizo ni kama vile istilahi zihusuzo majina katika familia: 'baba' 'mama' 'shangazi', na 'mjomba'. Kiuwiano, katika kundi zima la alama zenye uhusiano wa moja kwa moja na Kiswahili, alama zinazolazimika kuambatana na matumizi ya mdomo (kuashiria matamshi yake) ni 29.2%.

5. Uchambuzi na majadiliano ya matokeo

Mchango wa Kiswahili katika LAT unaweza kuchambuliwa kwa kuzingatia vigezo vikuu viwili, ambavyo ni, kwanza, jinsi Kiswahili kinavyochangia katika uundaji wa alama za LAT na, pili, jinsi kinavyochangia katika kujifunza na kuzifasiri alama. Uchambuzi huo unatolewa katika vifungu 5.1 na 5.2 hapa chini.

5.1. Mchango wa Kiswahili katika uundaji wa alama za LAT

Utafiti huu umeonyesha kuwa alama za LAT zilizo nyingi ni tanakali. Hata hivyo, hali hii ya utanakali haina msingi wowote na wala haitokani na Kiswahili. Hii ina maana kwamba, kizazi huunda alama zake mbalimbali kutokana na vigezo mbalimbali vya hali na mazingira yake anamoishi. Kwa mfano, katika alama zote zilizotafitiwa, ni asilimia 13% tu ya alama ambazo zilihusiana moja kwa moja na Kiswahili. Ingawa hatuwezi kukipuuza moja kwa moja kiwango hiki siyo muhimu sana kiasi cha kuweza kuathiri ukuaji na maendeleo ya LAT, hasa kwa wakati huu.

Tukiangalia pia upande wa alama zilizo angavu, tunaona kuwa uangavu wa alama hizo hauna msingi wowote katika ujuzi au maarifa ya mtu katika Kiswahili. Alama angavu zilizo nyingi ni ishara za kawaida kabisa ambazo mtu yeyote kutoka lugha nyingine yoyote, yaani asiye mswahili, anaweza kuzifasiri. Hii inamaanisha kuwa si lazima mtu kuwa na mashiko katika Kiswahili ili uweze kuzielewa alama hizo angavu. Kwa ujumla, alama hizo hupatikana zaidi katika nyanja mahususi za kisemantiki, kama vile, majina (mf. majina ya mahali, makabila) na siku za juma kama vile Jumatatu na Jumanne.

Matokeo ya utafiti yamedhihirisha pia kwamba alama ambazo ni tanakali (zilizo na zisizo dhahiri) pamoja na angavu zitakuwa zikiupoteza utanakali na uangavu wake jinsi siku zina-

vyopita. Hii ina maana kuwa baada ya vizazi kadhaa, watumiaji wa LAT hawataweza kutambua etimolojia ya utanakali wa alama hizo bila kuelezwa au kuzisoma katika taarifa za utafiti kama huu. Kwa hivyo, LAT inafuata msingi uleule wa kiasili katika ukuaji na kuendelea kwake kama lugha nyingine za alama zilivyofanya, k.v., Lugha ya Alama ya Marekani, yaani (ASL). Kwa maneno mengine, alama za LAT zitabadilika taratibu kutoka kwenye utanakali na uwakilishi kuwa alama nasibu.

5.2. Mchango wa Kiswahili katika kujifunza na kuzielewa alama za LAT

Utafiti umebainisha sababu tatu za kuwepo kwa matumizi ya Kiswahili katika shughuli za LAT. Sababu ya kwanza inatokana na kuwepo kwa haja ya matumizi ya mdomo kwa baadhi ya alama, yaani, kiziwi hutumia mikono yake kuonyesha alama na wakati huo huo huongezea pia maumbo ya mdomo kuashiria matamshi ya neno la alama hiyo kwa Kiswahili. Pili ni matumizi ya alama pamoja na kuzungumza; na tatu ni kutafsiri moja kwa moja toka Kiswahili kwenda kwenye LAT.

Tukianza na sababu ya kwanza, kuna mambo mawili yaliyobainika. Kwanza, imeonekana kuwa njia hii hutumika hasa kama mbinu ya kutofautisha alama mbili, au zaidi, zinazofanana kiumbo lakini zikiwa na maana tofauti. Mfano mzuri ni alama itumikayo kumaanisha "baba" na "mjomba" ambayo huonyeshwa kwenye kidevu. Kwa kuwa alama ni ile ile *moja*, na ni vigumu kutofautisha dhana hizo mbili kimatumizi, na bahati nzuri viziwi wanafahamu maneno yake kwa Kiswahili, basi wakaamua kuongezea maumbo ya mdomo ili kutofautisha alama hizo mbili. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa midomo hutengeneza umbo la neno bila ya muhusika kutoa sauti ya matamshi ya neno hilo. Pili ni kwamba ilithibitika kuwa kiziwi akiwasiliana na mtu asiye kiziwi, hutumia alama na pia kusema maneno mdomoni. Mbinu hii hutumiwa na viziwi hata kama wanaoongea nao ambao si viziwi wanazifahamu na kuzitumia alama. Mbinu hii hutumia zaidi matamshi ya maneno kwa sauti kuliko ile ya kwanza (ya kutofautisha alama moja na nyingine). Lakini kwa upande mwingine mbinu hii hutumiwa kwa nadra sana wakati viziwi wanapowasiliana wao kwa wao. Tumeitafsiri mbinu hii kama njia ya viziwi ya kuwapambanua watumia alama katika makundi mawili: watumia alama halisi (kama lugha yao) yaani viziwi wenyewe, na watumia alama walio pia wazungumzaji.

Sasa tuangalie sababu ya pili ya matumizi ya Kiswahili katika LAT. Imeonekana dhahiri kwamba viziwi walio wengi wanaweza kutumia alama na wakati huo huo kuzungumza, hasa wanapowasiliana na mtu asiye kiziwi. Kwa kiasi fulani, jambo hili liliibua mshangao, kwa kuzingatia dhana ya msingi kwamba lugha hizi mbili, LAT na Kiswahili zina miundo na mipangilio tofauti ya maneno. Swala hili linaturudisha kwenye swali letu la msingi la kama LAT ni lugha ya alama halisi au ni Kiswahili katika Lugha ya alama. Hata hivyo, jambo moja tuliloligundua ni kuwa wale wote waliopata ukiziwi baada ya kujua kusema ndio hasa wanaotumia mbinu hii zaidi kuliko wale waliozaliwa viziwi. Kwa hali hiyo, utafiti zaidi unahitajika ili kujua undani zaidi wa makundi haya mawili ya viziwi pamoja na kuzichambua na athari za umahiri wao katika lugha wazijuazo.

Sababu ya tatu kuhusu athari za Kiswahili katika LAT inatokana na uwezo na urahisi wa kutafsiri misemo ya Kiswahili katika LAT. Kuna misemo kadhaa katika Kiswahili ambayo haipotezi maana yake ya awali inapotafsiriwa moja kwa moja katika LAT. Mfano mzuri ni nahau na methali. Viziwi ambao wana uelewa mzuri katika Kiswahili inawawia rahisi kufasiri misemo hiyo neno kwa neno. Mfano mzuri ni nahau zifuatazo:

21. kumvunja mtu moyo = "kumkatisha mtu tamaa"

22. kula chumvi nyingi = "kuishi miaka mingi"

Misemo kama hiyo huchukuliwa kama ilivyo na kuhamishiwa katika LAT kwa tasfiri ya neno kwa neno kama 'tafsiri mkopo'. Kwa mfano, kila moja ya nahau hizo itakuwa na alama tatu kwa ajili ya maneno yake matatu. Hali kama hii inajitokeza sana katika LAT kwa sababu viziwi walio wengi nchini Tanzania hujifunza Kiswahili shuleni, kabla ya kujifunza rasmi na kuimudu LAT. Kwa hivyo, kwa kuzingatia nafasi ya Kiswahili katika jamii ya Tanzania, mazingira yanayomfanya mtoto ajifunze Kiswahili kabla ya LAT, au kujifunza lugha zote zinazomzunguka kwa wakati mmoja, yanatoa mwanya mkubwa wa Kiswahili kuiathiri LAT kwa njia mbalimbali.

6. Hitimisho na Mapendekezo

6.1. Hitimisho

Kulingana na matokeo ya uchambuzi wa data za misamiati mia tano, pamoja na majadiliano yaliyofanywa katika vifungu mbalimbali kwenye makala haya, tunahitimisha kwa kusema kuwa LAT ni lugha ya alama na siyo Kiswahili katika Lugha ya alama. LAT ni lugha huru, na haitokani na lugha zinazozungumzwa kama vile, Kiswahili, ingawaje Kiswahili kitaendelea kuiathiri, hasa kwa sababu lugha hizi mbili zinatumika katika mazingira ya kiisimu yanayofanana. Hata hivyo, LAT imefaulu kupunguza kasi ya athari za lugha nyingine kwake, hasa katika kiwango cha msamiati. Hali hii inamaanisha kuwa LAT inaweza kuhimili, ikasimama yenyewe na kuendelea bila Kiswahili. Hata hivyo, utafiti zaidi unahitajika, hasa kwa upande wa sarufi, ili kutoa majibu yaliyo thabiti.

6.2. Mapendekezo

Utafiti huu uliofanyika ni mwanzo tu, bado tafiti zinahitajika sana. Yapo maeneo katika LAT yanayohitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina, kufafanuliwa na kuchambuliwa zaidi ili kufahamu undani wa lugha hiyo na kisha kuiendeleza. Maeneo hayo ni: i) kuangalia kiwango cha usambaaji na kukubalika kwa LAT; ii) kukusanya na kuhifadhi alama zote za sasa kutoka mikoa yote ya Tanzania; iii) kutengeneza kamusi ya kisasa ya LAT; iv) kufanya uchambuzi wa sarufi ya LAT; v) kutafiti tofauti za kiisimu baina ya viziwi waliopata ukiziwi baada ya kupata lugha ya mazungumzo na wale waliozaliwa na ukiziwi. Tunaamini kuwa tafiti hizo na nyingine zikifanyika, polepole, LAT itaendelea na kuwa lugha inayotumiwa katika nyanja zote muhimu za jumuiya ya viziwi Tanzania.

Marejeo

Boyes-Braem, Penny. 2001. "Functions of mouthing component in the signing of the deaf and later learners of Swiss German Sign Language." Diane Brentary (ed.). *Foreign Vocabulary in Sign Languages: A Cross Investigation of Word formation*. London: Lawrence Erlbaum Associates Publishers.

CHAVITA/TAD. 1993. *The Tanzanian Sign Language Dictionary: Swahili–English–Sign Language*. Dar es Salaam: Advert International (T) Ltd.

Fromkin, V. A. & R. Rodman. 1993. *An Introduction to Language*. New York: Holt, Rinehart & Winston.

Humphries, T., C. Padden, and T. J. O'Rourke. 1985. *A Basic Course in American Sign Language*. Twelfth Printing, T. J. Publishers.

Joutselainen, Marjo. 1988. *A report on East African sign language seminar, Arusha, Tanzania: 29th August – 9th September 1988*. Finnish Association of the Deaf.

Kair, Debbie Sr. 1988. "My two years working with the Deaf in Tanzania: A reflection". *A report on East African sign language seminar, Arusha, Tanzania 29th August – 9th September 1988*. Finnish Association of the Deaf.

Klima, E. & U. Bellugi. 1979. *The Signs of Language*. Massachusetts: Harvard University Press.

Mreta, A. Y. & H. R. T. Muzale. 1999. *A report on the national workshop / seminar for CHAVITA leaders and members on the White Paper (No 1, 1998)*. Morogoro.

Mreta, A. Y. and H. R. T. Muzale. 2001. *A Research Report on 'The influence of Kiswahili on Tanzanian Sign Language*. Dar es Salaam: University of Dar-es-Salaam.

Possi, M. K. 1999. "Kiswahili kama lugha ya kufundishia wanafunzi viziwi katika shule za sekondari nchini Tanzania." *Kiswahili* (Journal of the Institute of Kiswahili Research) University of Dar es Salaam.